Shahaadah

(Kalimatu-tawheed)

أشهد أن لا إله إلا الله

و أشهد أن محمدا رسول الله

Maana Yake Na Sharti Zake

Shaykh Dr.Saleh As-Saleh (rahimahullaah)

Shahaadah

Kalima ya ‘eeman (tawheed)

أشهد أن لا إله إلا الله

و أشهد أن محمدا رسول الله

Ash-hadu an la ilaaha illal-laah
Wa Ash-hadu anna Muhammadan rasulullaah

Nashuhudia na nakubali ya kwamba hapana Mola
Apasae kuabudiwa kwa haki, isipokuwa Allaah
na Nashuhudia na nakubali ya kwamba Muhammad
ni Mtume wa Allaah.

Maana Yake
Na
Sharti Zake

Shaykh Dr.Saleh As-Saleh (rahimahullaah)
Imefasiriwa na manhajyasalafi.com

Kalima ya (tawheed) eeman

لا إله إلا الله محمد رسول الله

Ina maanisha nini?

Hii ndiyo asili ya nguzo (msingi) wa kwanza katika itiqadi (imani) ya Tawheed (Umoja na Upwekeshaji wa Allah). Allaah ni Mmoja katika Umola Wake, Allah ni Mmoja katika Uungu Wake (Yeye ndiye anastahiki Upweke wa kuelekezewa ibada) , na Allah ni Mmoja na ni Mpweke katika vitendo Vyake na katika Majina na Sifa Zake.
Mtu anapomkubali Allah kuwa ndiye Mola wa Haki na Yeye pekee ndiye Anayestahiki kuabudiwa ; basi ni lazima [vile vile kila mtu] akataye (na ajiepushe na akanushe) ibada zozote nyngine zinazofanywa (zinazoelekezwa) kwa mtu (au kitu) pasi na Allaah .

Hii ndio maana ya: ***la ilaaha illa-Allaah***: **"hapana Mola Apasae kuabudiwa kwa haki, isipokuwa Allaah".**

Kalima hii imestawi kwa kauli ya kukanusha na kauli ya kukiri (kukubali). Tamshi la: *'isipokuwa Allaah'* linathibitisha kuwa Allaah pekee ndiye Mungu wa Haki Anayestahiki kuabaudiwa.

Allaah ni Aliyekamili kwa Uadilifu, na ni Mwenye Hikma. Ametuumba na anataka tumjuwe na tumuabudu Yeye pekee. Hakutuwacha bila ya mwongozo. Hii ni sehemu katika sehemu ya Rehma Zake.
Yeye , Aliyetukuka , ametuma mitume na manabii (wote) kufikisha ujumbe mmoja : (ya kuwa) binaadamu ni lazima (atwii na) ajisalimishe kwa matakwa ya Mola wao Muumbaji , na wamuwaabudu Yeye peke Yake.

Huu ndio msingi wa al–Islam. Ni risala ile ile aliyoifikisha Adam, Ibraaheem, Moosa, 'Eesa na hatimaye mwisho Muhammad (sallahAllaahu alayhi wasallam) ; kwa watu wote mpaka siku ya Kiyama.
Hawa manabii na mitume walikuwa binaadamu walioumbwa [kama sisi].

Katika ujumbe wa mwisho uliotumwa (ukafikishwa) kwa binaadamu ni : kukubali na kukiri ya kuwa : *"Hapana Mola Apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah, na [kushuhudia na nakukubali] Muhammad kwa hakika ni Mtume wa Allaah."*

(Itikadi Na) Kalima hii ndio ufunguo wa pepo.
Lakini! Hakuna ufunguo usiokuwa na meno ama ncha (zake maalum). Ndio pale unaona ya kuwa ukija na ufunguo ulio na meno na uliochongwa sawasawa; mlango unafunguka. Lau kama si hivo ; mlango hautafunguka abadan!

Kwa hivo Yeyote yule anayetaraji na anayetaka kuingia peponi (na kujepusha na moto) kwa kalima hii ya ***"laa ilaaha illa-Allaah"*** **;** basi Inawajibika ya kuwa atimize masharti fulani ambayo ndiyo 'meno na mchongo' mahususan wa kalima hii [ambayo ni ufunguo wa pepo] .

Masharti hayo ni:

1. *Al-'Ilm* – Ilimu

Ilimu ya kumjuwa Allaah (tawheed), na ilimu ya mfumo, dhati na mbinu za ibada: ni muhimu kwa (dasturi) vitendo vya kiislamu pamoja na [kuwa ni muhimu katika] kuufahamu uislamu.

Ilimu ya manufaa ni ile yenye kukuelekeza katika kukana (kukataa) waungu wengine, na pia inakuelekeza katika kuamini na kufanya nia zako [za amali] ni kwa sababu ya Allah pekee (*al-ikhlaas*).

Allaah, Aliyetukuka anasema;

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مُتَقَلَّبَكُمْ وَمَثْوَاكُمْ

"Basi jua ya kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki ila Mwenyezi Mungu, na omba maghufira kwa dhambi zako na (dhambi) za waislamu[Waumini] wanaume na waislamu [Waumini] wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa."
(Soorat Muhammad, 47:19).

Mtume Muhammad (sallahAllahu alayhi wasallam) amesema;

"Atakayekufa akiwa ana juwa (ana ilimu ya sawasawa) ya kuwa Hapana Mola Apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah : ataingia Al-Jannah (peponi) ."

(Imekusanywa na Imaam Muslim)

2. *Al-Yaqeen* – Yakini

Kalima hii ya (*laa ilaaha illal-laah Muhammad rasulullaah*) ni lazima isemwe kwa ulimi na iaminiwe katika moyo ; bila ya shaka yeyote [kuhusu maana yake] .

Allaah , Aliyetukuka anasema ;

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أُوْلَئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ

"Hakika Wenye kuamini kweli kweli ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ; kisha wakawa si wenye shaka [kabisa], na wakapigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio wenye kuamini kweli."

(Sooratul Hujuraat, 49:15).

Mtume Muhammad (sallahAllahu alayhi wasallam) amesema;

"Nashuhudia na nakubali ya kuwa hapana Mola Apasae kuabudiwa kwa haki, isipokuwa Allah na [Nashuhudia na nakubali] ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah. Hakuna Mja wa Allaah yeyote atakaye kutana na Allaah [siku ya malipo] , ***ambaye hana shaka [juu ya kalima hii]*** *isipokuwa [Allaah] atamuingiza Al-Jannah (peponi) ."*

(Imekusanywa na Imaam Muslim)

3. *Al-Ikhlaas* – uthibitisho Na kutakasika Nia

Nia ya kuukubali Uislamu pamoja, na [nia ya] vitendo vyote (amali zote) ; ni LAZIMA [nia] iwe kwa sababu ya Allaah pekee.

Allaah , Aliyetukuka anasema ;

قُلْ إِنِّي أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ مُخْلِصًا لَّهُ الدِّينَ

“Sema: “Hakika [mimi] nimeamrishwa nimuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia Dini Yeye tu.”
(Soorah az- Zumar, 39:11).

Kwa hivyo mtu yeyote akiikubali na kukiri kalima hii ya (*laa ilaaha illal-Allaah Muhammad rasulullaah*) ; ni lazima iwe kwa sababu ya Allaah . Si kwa sababu ya mtu yeyote mwingine.

Ikhlaas (Usafi na kutakasika kwa Nia) ni kinyume cha shirk (kuwanasibisha wengine katika yale anayostahiki Allaah peke Yake; kama vile kuwategemea au kuwaabudu hao au kuwaabaudu hao pamoja Naye).

Yule ambaye anatamkaa kalima hii ya shahada ; kwa sababu ya kufaidika na vitu vya ki ulimwengu , basi hajakamilisha sharti hii ya kusafisha na kuthibitisha ibada [ziwe ni kwa sababu ya Allah] .
Na pia amekwisha shindwa kufuwata amri ya Allah Aliposema :

قُلِ اللَّهَ أَعْبُدُ مُخْلِصًا لَّهُ دِينِي

“Sema: “Mwenyezi Mungu tu namuabudu , kwa kumsafishia Yeye tu Dini yangu.”
(Soorat az-Zumar, 39:14)

Mtume Muhammad (sallahAllahu alayhi wasallam) amesema ;

*“….. kwa hakika Allaah Ame muharamishia moto , yule anayesema laa ilaaha illa-Allaah ; **kwa kutaraji kwa kauli hiyo [anayosema na kuiamini] Uso wa Allaah.” [yaani ikhlaas].***

(hadeeth imekubalika)

4. *As-Sidq* – kusadikisha (Usahihi)

Ukweli (uhalisi) unatengeza njia ya ufahamu ambao unaonufaisha kalima hii (*ya laa ilaaha illal-Allaah Muhammad rasulullaah*) . Humuongeza nguvu mtu na kumtimizia hima ya kutaka kupata ilimu ya kumjuwa Muumbwa wake, [naye ni] Allaah. Wanafiki hutamka kalima hii , lakini wakaficha kuipinga kwao na kutoamini kwao katika nyoyo zao :

سَيَقُولُ لَكَ الْمُخَلَّفُونَ مِنَ الْأَعْرَابِ شَغَلَتْنَا أَمْوَالُنَا وَأَهْلُونَا فَاسْتَغْفِرْ لَنَا يَقُولُونَ بِأَلْسِنَتِهِم مَّا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ قُلْ فَمَن يَمْلِكُ لَكُم مِّنَ اللَّهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ بِكُمْ ضَرًّا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ نَفْعًا بَلْ كَانَ اللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا

Watakuambia wale mabedui waliokaa nyuma (wasende vitani wala hawana udhuru wowote;watijadai ktuo udhuru waseme) : “Mali zetu na watu wetu walitushughulisha, basi tuombee msamaha.” Wanasema kwa ndimi zao (maneno) yasiyo kuwamo katika nyoyo zao. Sema: “Ni nani awezaye kukusaidieni chochote kwa Mwenyezi Mungu akitaka Yeye kukudhuruni au akitaka kukunufaisheni?” Bali Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda yote.

(Soorat ul- Fath, 48:11)

Moyo ni kama mfalme, na viungo ndio majeshi.
Mtume Muhammad (sallahAllahu alayhi wasallam) amesema ;

“Kwa uhakika! Katika mwili kuna pande la nyama; litakapokuwa zuri, basi mwili wote huwa mzuri (mtu huwa mwema). Na likiwa (ovu) lenye ufisadi; basi mwili wote utakuwa muovu (mfisadi). Kwa hakika (pande hilo la nyama) ni moyo.”

[kipande cha hadeeth iliyokusanywa na Bukhaaree & Muslim]

Mapenzi ya Allaah yakistawi katika moyo wa mtu ; basi uaminifu na usahihi[wa imani] hustawi [na hujaa] katika moyo.
Lakini hawaa (matamanio) yakiufikia moyo; njia za ufisadi na unafiki zinafunguka, na mtu anaweza kusema (kutamka) yale yasiyomo katika moyo wake [asiyoyaamini].

Moyo ulio stawi na wenye utulivu [wa imani] ni ule ambao umeepukana na:

a) Kumshirikisha mtu yeyote / kitu chochote katika kumuabudu Allaah
b) Kibri na majivuno na ufahari
c) Wivu na uhasidi
d) Shari (kinyonge)
e) Kupenda maisha ya dunia
f) Kupenda uongozi Na utawala
g) Hawaa (matamanio)
h) Bid'ah (uzushi katika dini)

Huu ndio moyo uliotimiza kuikubali na kukiri kalima ya *shahaadah .* Hii ndiyo inajulikana katika Qur'an kama : ***"Al-Qalb as-Saleem,"*** `moyo uliosalimika , wenye utulivu na uliokamilika [katika kukubali eeman] .' Na hichi ndicho kitu chenye thamani kubwa siku ya Kiyama :

يَوْمَ لَا يَنفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ. إِلَّا مَنْ أَتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ

"Siku ambayo [kwamba] hayatafaa mali wala watoto. Isipo kuwa mwenye kuja kwa Mwenyezi Mungu na moyo safi; (huyu ndiye atakayepata ya kumfaa)."

(Soorah ash-Shu'araa', 26: 88-89)

5. *Al-Mahabbah* – Mahaba (Mapenzi)

Mahaba Ina maanisha:

a) Kumpenda Allaah na Mtume Wake , Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) : kuliko kitu chochote kingine.

b) Kupenda mambo yanayopendwa na Allaah na Mtume Wake (sallaAllaahu alayhi wasallam).

c) Kuchukia mambo yanayochukiwa na Allaah na Mtume Wake (sallaAllahu alayhi wasallam): katika mambo yote.

Mtume Muhammad (sallahAllahu alayhi wasallam) amesema ;

"Yeyote atakaye kuwa na mambo matatu [haya] ataonja [atafurahia] utamu wa imani:

***- Mtu ambaye Allaah na Mtume Wake (sallaAllahu alayhi wasallam) ni bora na anawapenda zaidi kuliko kitu chochote kingine** ;*
***-** awe anampenda mtu kwa sababu ya Allaah pekee (yaani kumpenda mtu mwingine sababu ya dini na kumridhisha Allaah pekee Yake) ;*
- awe anachukuia [na kuhofia] kuregea katika kufr [kuritadi] baada ya kuwa Allaah amemuokowa kutokana nayo [hiyo kufr], na awe [hali kadhalika] anachukia [na anahofia] awe atatupwa [atatiwa] motoni [jahannam]. "

(Imekusanywa na Al-Bukhaaree & Muslim)

Mahaba ya kumpenda Allaah na Mtume Wake, Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam): ni lazima yawe [pia] ni katika kufuata amri Zao.

Hii inakanusha kufuata wazushi [ahlul bid'a] na uzushi wao , wale ambao wanaongeza na wanazusha mifumo na njia ambazo hazimo katika mafundisho ya uislamu ; kama vile mambo ya ki sufi na migawanyo wanayoyaita 'tareeqa (njia)' , ambayo [haya yote] hayana uhusiano wowte na uislamu[wa sawa]. Wana tukuza mashekhe wao wa kisufi na viongozi (aqtab) wao kama ni watukufu (wasio binaadamu wa kawaida). Vile vile , ma *Raafidhah* (mashi'a) wanamtukuza 'Ali na watu wengine wa familia ya mtume (sallaAllaahu alayhi wasallam) wakawafanya na utukufu (usio wa kibinaadamu) , mpaka wakaawaomba wao pamoja na [Allaah] , ama pasi na kumuomba Allaah!

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ اللّهِ أَندَاداً يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللّهِ وَالَّذِينَ آمَنُواْ أَشَدُّ حُبًّا لِّلّهِ وَلَوْ يَرَى الَّذِينَ ظَلَمُواْ إِذْ يَرَوْنَ الْعَذَابَ أَنَّ الْقُوَّةَ لِلّهِ جَمِيعاً وَأَنَّ اللّهَ شَدِيدُ الْعَذَابِ

"Na katika watu kuna wanao fanya waungu wasio kuwa Mwenyezi Mungu. Wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walio amini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana. Na laiti walio dhulumu (nafsi zao) wanaijua (balaa itakayowapata) watakapo iona adhabu(siku hiyo ya Kiyama) , kuwa nguvu zote ni za Mwenyezi Mungu(siku hiyo- hakuna masanamu wakuwasaidia wala mengineyo) na kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu!"

(Soorat ul-Baqarah, 2:165)

Katika hadeeth (hii), Abdullah bin Mas'ud (radhiyaAllahu anhu) asema:

" Alisema mtume (sallaAllahu alayhi wasallam) kauli moja nami [Abdullaah bin Mas'ud] nikaongeza nyengine ; Alisema mtume (sallaAllahu alayhi wasallam) :

'Atakayekufa na awe huomba (huabudu) kitu chengine pasi na Allah , kumfanyia mpinzani Allaah [katika maombi (ibada) yake] ; ataingia motoni.

Nami nikasema: "atakayekufa hali ya kuwa haombi kitu chochote kingine (kuwa ndiye mungu wake) kama mpinzani wa Allaah; ataingia Al-Jannah (peponi)."

(Imekusanywa na Al-Bukhaare)

Mahaba ya kumpenda Allaah na Ujumbe Wake wa Uislamu unahusiana na ilimu ya kumjuwa Allaah na kujuwa Majina Yake na Sifa Zake (hii ni tawheed).
Ilimu ya kumjuwa Allaah ikizidi, na mahaba ya kumpenda Allah huongezeka. Hii humfanya muu'min awe na hamu ya kukutana na Allaah , kumuona [Allah] , na kusikiza maneno Yake [Allaah] katika akhera .

Hili ndio huwa lengo lake [muu'mini], na kwa hivyo mapenzi ya kupenda maisha na starehe za dunia hupungua na kufifia. Hivyo uchangamfu na mori [ya ibada] huongezeka, ikawa lengo ni kwa Allaah, Muumba wake.

Hautojifunga [moyo wa muu'mini] katika kushika njia yeyote nyengine isipokuwa ile njia yenye kulekeza katika kumtii na kujisalimisha kwa Allaah peke Yake.
Mtu huwa na bidii na jitihada ya kushikamana na kufuata maamrisho ya Allah , kwa uwezo wake wote.

Haya ndio huleta furaha ya kikweli; katika maisha haya [ya dunia] na akhera.

6. *Al-Inqiyaad* – Utiifu na Ufuwataji

kalima ya shahada hukamilika kwa kumtii Allaah na kumtii Mtume Wake, Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) ; kwa kujikinga na kujiepusha na yale yaliyokatazwa na Allaah :

وَمَن يُسْلِمْ وَجْهَهُ إِلَى اللَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَى وَإِلَى اللَّهِ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ

“Na ajisalimishaye uso wake kwa Mwenyezi Mungu, na hali ya kuwa anafanya mema, bila shaka [huyo] amekwisha kamata fundo lilio madhubuti. Na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu.”
(Soorat-ul Luqman, 31:22).

Utiifu na ufwatajii huu wa kalima cha shahada ni lazima uwe bila ya wasiwasi na bila ya kusitasita. Bali ni jambo la utiifu na ufuwataji wa kikamilifu . Hii imeelezwa vizuri katika maneno ya Allaah:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا

“Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke ; Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri [katika jambo] , kuwa na khiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi (kabisa).”
[Soorat ul-Ahzaab, 33:36].

Hukmu [maamrisho] ya Allaah na ya Mtume Wake ; hayapimwi wala kuchunguzwa na binaadamu. Ujumbe huo ni wahyi.

Yote yaliyomo [maamrisho na makatazo] ni ya kumnufaisha binaadamu.

Kwa hivyo utiifu na kufuwata uislamu ni kwa faida ya kila mtu mwenyewe.

7. *al-Qubool* – kukubali na kuridhika

Haitoshelezi kujuwa utukufu wa uislamu na kuwa uislamu ndiyo Haki, bali kujuwa huku lazima kupatikane kwa kupitia; kukubali, kuridhika na unyenyekevu.

Kushikamana na maana [na mafundisho] ya kalima hii; humweka mbali muu'min kutoka na kibri, majivuno na utakabari:
[Kuhusu ma kuffar wa ma quraysh, Allaah asema] :

إِنَّهُمْ كَانُوا إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ

"Wao walipo kuwa wakiambiwa "[Laa ilaaha illa 'Llahu] Hakuna aubudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu ," walikuwa wakikataa."
(Soorat as-Saafaat, 37:35).

Muislamu lazima ajuwe kuwa kalima hii ya shahaadah ina kataza [inapinga]; ushupavu wa kufuata (kiuiga) bila ya uongozi wa sawa , na kuwa [kalima hii ya shahaadah] ina elekeza kukubali mafundisho ya uislamu kupitia kwa fahamu ya wale waliokuwa katika njia ya sawa (sunnah).
Hawa ni maswahaba (radhiyaAllahu anhum ajma'in), na wale wanaofuwata mwenendo wao; mpaka siku ya mwisho.

Hii njia [ya uongofu], inajulikana kama njia ya ***as-Salafus-Saalih*** (watu wema waliopita).

Mtume Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) ametoa mithali nzuri ilioje ; kuhusu wale wanao kubali na wale wanao kataa uongofu na mafundisho ya uislamu , amesema (sallaAllahu alayhi wasallam) :

" Mfano wa uongofu [huu] na ilimu [hii] aliyonituma nayo Allaah ; ni mfano wa mvua nyingi inayoshuka katika ardhi , kukawa katika ardhi hiyo mchanga wenye rutba ukachukuwa maji yale ya mvua na ukastawisha mimea na manyasi kwa wingi.

Na kipande chengine [cha ardhi] kikawa kigumu kikazuulia maji yale yakawafaa watu kwa kunywa , kunywisha wanyama wao na kwa kupanda mimea .

Na kipande chengine [cha ardhi] kikawa parama [tasa] hakizuwii maji wala hakistwashi mimea, (kikawa kipande hichi cha ardhi, hakimnufaishi yeyote).

Huu ndio mfano wa yule aliye na ujuzi wa ilimu ya dini ya Allaah na akanufaika (kupitia ilimu hiyo) , ambayo Allaah amenitumia [mtume] ,akajifundisha na akafundisha wengine . Na mfano wa mwisho, ni wa yule asiyejali [ilimu hiyo] , na asiyekubali uongofu ambao Allaah ameutuma [kwa watu] kupitia mimi (huyu ndiye mfano wake kama ardhi parama isiyo kuwa na manufaa). "

[Imekusanywa na Al-Bukhaare]

Kipande cha pili cha Shahaadah

محمد رسول الله

Muhammad ni Mtume wa Allaah

Hii ndiyo sehemu ya pili ya kalima cha shahaadah. Ni kukubali na kuamini kuwa Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) ni mtume wa mwisho wa Allaah. Hii inamaanisha [kuamini kuwa]:

1. Yote aliyotueleza Allaah kuhusu Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) ni ukweli

لَقَدْ جَاءكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِالْمُؤْمِنِينَ رَؤُوفٌ رَّحِيمٌ

“Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. (Na) Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.”

(Sooratu t-Tawbah, 9: 128).

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَاهِدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا. وَدَاعِيًا إِلَى اللَّهِ بِإِذْنِهِ وَسِرَاجًا مُّنِيرًا

“Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kwa yakini Sisi tumekutuma, (tumekuleta uwe) shahidi na (mbashiri) mtoaji wa habari nzuri , na Mwonyaji, Na uwe mwitaji (wa watu) kwa Mwenyezi Mungu, kwa idhini Yake, na (uwe) taa yenye kutoa nuru.”

(Soorat ul-Ahzaab, 33: 45-46)

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَى إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَاء رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا

“ Waambie: “Bila shaka Mimi ni binaadamu kama nyinyi(isipokuwa nimeltewa wahyi tu!). Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Anayapenda kukutana na (jaza ya) Mola Wake (basi) naafanye vitendo vizuri, wala asimshirikishe yoyote katika ibada ya Mola Wake.”

(Qur'an, soorat al-Kahf, 18:110)

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَى رَجُلٍ مِّنْهُمْ أَنْ أَنذِرِ النَّاسَ وَبَشِّرِ الَّذِينَ آمَنُواْ أَنَّ لَهُمْ قَدَمَ صِدْقٍ عِندَ رَبِّهِمْ قَالَ الْكَافِرُونَ إِنَّ هَـــذَا لَسَاحِرٌ مُّبِينٌ

**“Je! Ni ajabu kwa watu ya kwamba tumemfunulia (tumemletea wahyi) mtu miongoni mwao kuwa: “Waonye watu, na wabashirie wale walio amini ya kuwa watakuwa na cheo kikubwa mbele ya Mola wao?”
Wakasema makafiri: “Hayakuwa haya ila ni kiini macho!”**
(Sooratu Younus, 10: 2)

قُل لاَّ أَمْلِكُ لِنَفْسِي نَفْعًا وَلاَ ضَرًّا إِلاَّ مَا شَاء اللّهُ وَلَوْ كُنتُ أَعْلَمُ الْغَيْبَ لاَسْتَكْثَرْتُ مِنَ الْخَيْرِ وَمَا مَسَّنِيَ السُّوءُ إِنْ أَنَاْ إِلاَّ نَذِيرٌ وَبَشِيرٌ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

“Sema : Sina mamlaka ya kujipa nafuu wala kujiondolea madhara, ila apendavyo Mwenyezi Mungu ; Na lau kama ningalijua ya ghaibu ninge jizidishia mema mengi , wala isingeli nigusa dhara ; Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mtoaji wa habari njema (mbashiri) kwa watu wanao amini.”
(Soorat ul-A’raaf, 7:188).

2. Ni lazima tumuabudu Allah kupitia mfumo aliyoufundisha Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam)

Kumtii Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) ni Amri kutoka kwa Allaah :

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

“Na anacho kupeni Mtume chukueni(basi pokeeni) , na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na muogopeni Mwenyezi Mungu ; Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.”
(Soorat ul-Hashr, 59:7)

Maana ya aya hii Imeelezwa vizuri sana katika hadeeth hii:

Alituhadithia 'Alqama ; Abdullaah (bin Mas'ud) alisema :

"Allaah amewalaani wanawake wenye kuwachora watu michoro ya (tattoo) , na wale wanawake wanaochorwa michoro ya tattoo) , na wanawake wanozitoa [wanaozinyoa au kuzipunguza] nywele za uso [nyusi] na wale wenye kufanya hivyo, na [wanawake] wanao tengeza mwanya baina ya meno yao ili waonekane wazuri zaidi ; hivyo [wote hao] hubadilisha maaumbile ya Allah."

Kauli yake hii (bin Mas'ud) ikamfikia mwanamke mmoja katika kabila la Bani Asd aitwaye Um Ya'qub , huyu akaja (kwa bin Mas'ud) akasema : " imetufikia sisi kuwa wewe (bin Mas'ud) una walaani wanawake [wenye kufanya] kadha wa kadha ?"

Akasema (bin Mas'ud): " Je , kwa nini nisi walaani , waliyo laaniwa na mtume (sallaAllahu alayhi wasallam) , na wamelaaniwa katika kitabu cha Allaah (Qur'an)."

Akasema yule mwanamke: "nimeisoma (Qur'an) yote, lakini sikuona hayo unayosema [ya kuwalaani hawo wanawake]."

Akasema (bin Mas'ud): "Kwa hakika kama umeisoma (Qur'an yote) basi, umeipata [hiyo hukmu ya kuwalaani wanawake hao…] ; kweni wewe hukusoma :

"Na anachokupeni Mtume basi pokeeni , na anacho kukatazeni jiepusheni nacho."

Akasema yule mwanamke: " Ndio nimeisoma."

Akasema (bin Mas'ud): " Kwa hakika Mtume amekataza mambo hayo [ya tattoo, kutengeza nyushi…]."

Akasema yule mwanamke: " lakini mimi nimemuona mke wako [bin masu'd] akifanya mambo haya ? "

Akasema (bin Mas'ud): "nenda ukamtazame ,[umwangalie kama anafanya hayo]."

Akaenda [mwanamke yule], akamtazama mkewe bin masu'd ; lakini hakupata kitu chochote cha kusaidia sababu yake .

Hapo akasema (bin masu'd): "angalikuwa [mke wangu] kama ulivyosema [kuwa anafanya mambo hayo ya laana] , basi kwa hakika nisingekaa naye [ningekuwa nisha muwacha] ."
(Imekusanywa na Al-Bukhaare).

[Dalili nyengine ya kuonyesha ulazima wa kufuwata Sunnah :]

مَّنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللّهَ وَمَن تَوَلَّى فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا

“Mwenye kumt'ii Mtume basi ndio amemt'ii Mwenyezi Mungu (kwani anayoaamrisha Mtume yanatoka kwa Mungu) .Na anaye kengeuka (anajidhuru mwenyewe) , hatukukupeleka wewe kuwa mlinzi juu yao (wakipotea hulaumiwi wewe).”

(Soorat un-Nisaa’, 4:80)

Na Mtume (sallaAllahu alayhi wasallam) amesema:

“Mwenye kunitii [kunifwata], amemtii Allaah. Na mwenye kuni asi [asinifuwate] , basi amemuasi Allah . Na mwenye kumtii kiongozi (amir) niliyemchaguwa, amenitii mimi. Na mwenye kumu asi kiongozi huyo, basi ameni asi mimi. ”

(Imekusanywa na Al-Bukhaare)

Pia amesema (sallaAllaahu alayhi wasallam) :

“Ummah wangu wote utaingia peponi isipokuwa wale wanaokataa.” Wakasema (maswahaba), ‘Ewe Mtume wa Allaah, ni nani atakayekataa!? ’
Akasema Mtume* (sallaAllaahu alayhi wasallam)*: “yeyote atakaye ni tii [atakaye fwata sunnah] ataingia peponi , na yeyote atakaye ni asi [asifwate amri zangu] , huyu ndiye aliyekataa[kuingia peponi].”

(Imekusanywa na Al-Bukhaare)

Mambo yanayoeleza ibada ya Allaah , utiifu na nidhamu , tabia njema , maamrisho , nasiha , mambo yaliyo kubaliwa , na mambo yaliyo sisitizwa kama yaliyovyo elezwa na Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) ; kwa ujumla [mambo haya yote] yanaitwa ***Sunnah***.

Hii ***Sunnah*** imeteremshwa kusistiza na kuelekeza katika kuelewa dini ya uislamu; [na ni] Kinyume ya mambo ya upotofu na uzushi (bid’a).

Hii ***Sunnah*** ni Wahyi kutoka kwa Allaah , wala si fikra , ama mipango ama matamanio ya Mtume (sallaAllaahu alayhi wasallam):

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَى. إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَى

“Wala hasemi (hatamki) kwa matamanio (ya nafsi yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila ni Wahyi ulio funuliwa (kwake).”

(Soorat un-Najm, 53 : 3-4)

Kwa hivyo utiifu kwa Sunnah ya Mtume (sallaAllaahu alayhi wasallam) ni utiifu kwa Allaah.

Haitakikani kuwepo na upinzani wala ubishi katika kufwata Sunnah ya Mtume (sallaAllahu alayhi wasallam).
Ni lazima Mtume (sallaAllahu alayhi wasallam) awe ndiye hakimu (mwamuzi) katika mambo yote. Kama vile Allah alivyoamrisha wazi wazi :

فَلاَ وَرَبِّكَ لاَ يُؤْمِنُونَ حَتَّىَ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لاَ يَجِدُواْ فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُواْ تَسْلِيمًا

“ La ! Naapa kwa (haki ya) Mola Wako ! Wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa , na wanyenykee kabisa.”

(Soorat un-Nisaa’, 4:65).

لَا تَجْعَلُوا دُعَاء الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ كَدُعَاء بَعْضِكُم بَعْضًا قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ الَّذِينَ يَتَسَلَّلُونَ مِنكُمْ لِوَاذًا فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa nyinyi kwa nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu Anawajua miongoni mwenu wale waondokao kwa utoro wakujificha. Basi wajihadhari wale wanao khalifu amri Yake, Usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu (chungu) iumizayo.”

(Soorat un- Noor, 24:63).

Mtume (sallaAllahu alayhi wasallam) amesema:

"Yeyote atakayefanya jambo ambalo halimo katika mfumo wa amri (uislamu) yetu , [jambo hilo] lita kataliwa."

(Imekusanywa na Muslim & Al-Bukhaaree kupitia maneno mengine)

Sunnah ya Mtume (sallaAllaahu alayhi wasallam) kwa hakika ina hifadhiwa kama vile Allaah alivyo ahidi kuokowa uislamu kutokana na uharibifu na uovu wa ki binaadamu.

Kufuata ***Sunnah*** ya Mtume (sallaAllahu alayhi wasallam) ndio uhakika wa kukiri na kuikubali kalima hii ya: **"MUHAMMAD NI MTUME WA ALLAAH":**

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

"Sema: "Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni (mimi) ; (hapo) Mwenyezi Mungu atakupendeni na (atakufutieni) atakughufurieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghufira na Mwenye kurehemu."

(Soorat aal-'Imraan, 3:31)

MUKHTASARI

Kalima ya kukubali kuwa Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) ni Mtume wa Allaah ; ni sehemu muhimu sana ya imani . Ni lazima tumuamini [na tumfuwate] Muhammad (sallaAllaahu alayhi wasallam) katika mambo yote aliyo tuambia kuhusu uislamu.
Yeye (sallaAllahu alayhi wasallam) ni lazima afuwatwe katika amri zote alizotuambia tufanye , na vile vile ni lazima tujiweke mbali na makatazo yote aliyokataza.

Utiifu kwa Muhammad (sallaAllahu alayhi wasallam) ni utiifu kwa Allaah.
Ametuwachia [amri zote ya] yote yatakayo tupeleka Al-Jannah (peponi); Na ametu tahadharisha na kutuonya na yote yale yanayompeleka mtu kwenye moto.

Walhamdulillaahi Rabbil 'aalameen.